MUHTASARI WA KIKAO CHA BARAZA MAALUM LA MADIWANI KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA WILAYA YA TANDAHIMBA TAREHE 28/09/2016

A: WAJUMBE WALIOHUDHURIA:

1.	Mh. Namkulya S. Namkulya	-Kata ya Mihambwe	-Mwenyekiti
2.	" Issa Nasoro Kalumbe	-Kata ya Mahuta	-Mjumbe
3.	" Ngerezani Bakari Musa	-Kata ya Kitama	"
4.	" Kawasaki Lipangati	-Kata ya Mnyawa	"
5.	" Simba Nasoro Hashimu	-Kata ya Naputa	"
6.	" Chimale S. Abdallah	-Kata ya Lukokoda	"
7.	" Sharafi Dihoni Hamisi	-Kata ya Malopokelo	"
8.	" Mtimbuka K.Ramandani	-Kata ya Nambahu	"
9.	" Jamali M.Mtima	-Kata ya Namikupa	"
10.	" Ally D. Nantindu	-Kata ya Michenjele	"
11.	" Nembo H. Mchola	-Kata ya maundo	"
12.	" Ahmadi A. Ndende	-Kata ya Mkoreha	"
13.	" Ashura m. Ngope	-Kata ya Mchichira	"
14.	" Ramadhani S. Ulaya	-Kata ya Milongodi	"
15.	" Mohamedi T. Ussi	-Kata ya Kwanyama	"
16.	" Selemani Y. Chambengela	-Kata ya Litehu	"
17.	" Ismail S. Chipoka	-Kata ya Ngunja	"
18.	" Zainabu H. Mpota	-Kata ya Mkonjowano	"
19.	" Alafa T. Nakatanda	-Kata ya Mkwiti	"
20.	" Ayubu Mohamedi	-Kata ya Lyenje	"
21.	" Rashidi N. Mtima	-Kata ya Chingungwe	"
22.	" Mfaume H. Abdallah	-Kata ya Miuta	"
23.	" Mkwahe M. Milembu	-Kata ya Chaume	"
24.	" Salumu A. Mnyongo	-Kata ya Dinduma	"
25.	" Abdallah H. Ponela	-Kata ya Luagala	"
26.	" Likapa J.Nangololo	-Kata ya Mndumbwe	"
27.	" Hamisi B. Nayowela	-Kata ya Tandahimba	"
28.	" Fakihi M. Mwango	-Kata ya Mdimba	"
29.	" Yusufu B. Nampoto	-Kata yaMkundi	"
30.	" Asha R. Tebwa	-Viti Maalum	"
31.	" Halima Tamatama	-Viti Maalum	"
32.	" Huduma S. Mnoda	-Viti Maalum	"
33.	" Hadija S. Mnihwika	-Viti Maalum	"
34.	" Shamia M. Kaisi	-Viti Maalum	"
35.	" Fidea A. Hittu	-Viti Maalum	"
36.	" Asia A. Likoba	-Viti Maalum	"
37.	" Rehema C. Liute	-Viti Maalum	"
38.	" Hawa M. Ramandani	-Viti Maalum	"
39.	" Amina A. Simba	-Viti Maalum	"
40.	Ndg Ahmada Suleiman	-Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)	Katibu

B: **WAJUMBE WASIOHUDHURIA**

1. “ Makuyeka B. Salum -Kata ya Chikongola -Kwa taarifa
2. “ Katani A. Katani -Mbunge- Tandahimba -Kwa taarifa
3. “ Mawazo S. Mbombenga -Kata ya Nanhyanga -Kwa taarifa
4. “ Amina Issa Mpota -Viti Maalum -Kwa taarifa

C: WAKUU WA IDARA NA VITENGO WALIOHUDHURIA

1. Ndg. Ally H. Machela -Mweka Hazina (W)
2. “ Sosthenes Luhende -Afisa Elimu Sekondari (W)
3. “ Mzenga T. Mzenga -Afisa Elimu (W)
4. Eng. Peter Malekia -Mhandisi wa Maji (W)
5. “ Salum Makinda -Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (W)
6. Ndg: Samson Kapange -Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi (W)
7. “ Faustine Pamba -Kny: Mganga Mkuu (W)
8. “ Constantine J. Kasese -Kaimu Afisa Mipango (W)
9. “ Lazaro Matoke -Kaimu Afisa Utumishi (W)
10. “ William Kongola -Mkaguzi wa ndani wa Hesabu
11. “ Carmichael Cipembe -Kaimu Afisa Utamaduni
12. “ Aloyce J. Massau -Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii
13. “ Mpangala P.N -Kaimu Afisa Ardhi, Maliasili na Mazingira (W)
14. “ Haroun Kisimba -Kaimu Afisa Kilimo,Umwagiliaji na Ushirika (W)
15. “ Zuberi Sarahani -Mwanasheria
16. “ Protas Muhanuzi -Afisa Manunuzi
17. “ Ismaely Mbilinyi -Mratibu wa TASAF
18. “ James C. Chitumbi -TEO Tandahimba
19. “ Nassib Namkuna -TEO- Mahuta
20. “ Joseph J. Mongi -Afisa TEHAMA
21. “ Ally Sembe -Kaimu Mratibu wa UKIMWI
22. “ James Mussa -Afisa Ushirika
23. “ Hamidu Mponda -Afisa Biashara
24. “ Suleiman Fumao -Mhasibu

D: WAALIKWA

1. Ndg: Eriko Amon -Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa Mtwara
2. “ Tonindo Mabele - Mkaguzi Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa Mtwara
3. “ Manzebele Said - Ofisi ya Afisa Usalama (W)
4. “ Bernad J. Osiah -Kny: Afisa Tarafa Litehu

E: SEKRETARIETI

1. Mohamedi Namkuva
2. Christian Mazuge
3. Sofia S. Nanjota

MUHT. NA. 01/2016/2017- KUFUNGUA KIKAO
Katibu alieleza kuwa kikao ni maalum kwa ajili ya kupitia hesabu za Halmashauri kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2016 na kisha alimkaribisha Mwenyekiti afungue kikao. Mwenyekiti alifungua kikao saa 06:27 mchana.

MUHT. NA. 02/2016/2017-KUPITIA TAARIFA YA FEDHA ZA HALMASHAURI YA WILAYA TANDAHIMBA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA JUNI 30, 2016.
Mweka Hazina (W) aliwasilisha taarifa ya fedha za Halmashauri ya Wilaya Tandahimba kwa mwaka wa fedha ulioishia juni 30, 2016 kama ifuatavyo:-

1. Mizania ya mwaka 2015/2016
Mpaka kufikia mwishoni mwa mwaka 2015/2016 rasilimali za Halmashauri za muda mrefu na mfupi zilikuwa na thamani ya jumla ya Sh 28,128,926,026/= wakati dhamana na dhima ya muda mrefu na mfupi ilikuwa na thamani ya Sh 9,835,543,668/= ongezeko la rasilimali za Halmashauri limetokama na Halmashauri kutekeleza miradi mbalimbali yenye mwelekeo wa rasilimali za kudumu pamoja na ununuzi, utengenezaji wa madawati na ujenzi wa maabara, nyumba, madarasa pamoja ofisi za watendaji wa kata.

2. Taarifa ya mapato na matumizi kwa mwaka 2015/2016
Halmashauri ilikusanya kutoka vyanzo vyake (own source) jumla ya Sh 3,553,854,839/= huku sehemu kubwa ikiwa ni makusanyo ya ushuru wa korosho, pia Halmashauri imepokea fedha za ruzuku na wafadhili jumla ya Sh 25,470,857,714/= na kutumia Sh 27,284,709,091/= sehemu kubwa ya matumizi haya ikiwa ni mishahara na matumizi yote ya kawaida na miradi ya maendeleo.

3. Taarifa ya Mtiririko wa fedha kwa mwaka 2015/2016
Mtiririko wa fedha kwa kuanzia kiwango cha ziada/albaki ya mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2016 ilikuwa kama ifuatavyo:-

• Uzidifu wa fedha kwa mtaji endesheo	2,639,564,125
• Fedha iliyotumika katika uwekezaji	(1,694,159,157)
• Ongezeko la fedha kutokana na ufadhili	393,178,867
• Ongezeko la fedha kwa mwaka 2015/2016	1,338,583,835
• Salio/Bakaa iliyokuwepo benki tarehe 1/7/2015	222,013,021
• Salio/Bakaa iliyokuwepo benki tarehe 30/6/2016	1,560,596,856

MAELEZO YA HALI YA FEDHA
A. MIZANIA
1. Fedha taslimu
Fedha taslimu imeongezeka kutoka Sh 0.222 bill mwaka 2015 mpaka Sh 1.560 bill 2016 ikitokana na kutolipwa kwa miradi ambayo bado inaendelea kutekelezwa.

2. Wadaiwa
Wadaiwa wameongezeka kutoka Sh 2,015,856,855 mwaka 2015 mpaka Sh 2,073,807,423. Hii imesababishwa na kuongezeka kwa mikopo ya vikundi vya vijana

na wanawake, hata hivyo hakukuwepo na urejeshaji wowote ule wa madeni ya vyama vya msingi vya ushirika kutokana na deni la ushuru wa miaka ya nyuma.

3. Malighalani.
   Mpaka tunafunga hesabu za mwisho kulikuwepo na mafuta, madawa, vifaa vya ofisi na shajala stoo kwa pamoja vikigharimu Sh 278,605,120

4. Rasilimali zinginezo
   Rasilimali zingine hazikuongezeka wala kupungua kwani zilisalia kiasi kilekile cha Sh. 127,541,300 ikiwa ni mchango kwenye kitega uchumi Taifa cha ALAT Dodoma.

5. Kitega uchumi cha ushirikiano (Investments in associates)
   Halmashauri imewekeze 453,686,046 kwa kununua hisa kwenye benki ya wananchi Tandahimba (TACOBA)

6. Majengo, mitambo na Vifaa
   Kwa mwaka 2015/2016 Halmashauri imefanikiwa kuongeza majengo, mitambo na vifaa kwa kiasi cha Sh 1,300,980,290 ambazo zimetokana na mapato ya ndani na Sh 393,178,867 zilizotokana na ruzuku toka serikalini na wafadhili, pia halmashauri imepokea msaada wa gari moja aina ya Totota Land Cruiser hard top ambalo linatumiwa na idara ya elimu msingi kutoka kwa 21st Century pamoja na masaada wa madawati kutoka kwa NMB, TANECU na Maliasili.

7. Wadai (payables)
   Wadai wamepungua kutoka kiasi cha Sh 627 mill hadi 170 mill kutokana na halmashauri kurejesha fedha za CHF ambazo zilikopwa kwa mwaka wa nyuma , huku kukiwa na ulipaji mkupwa wa madeni ya wazabuni na wakandarasi pia kupungua kwa madeni ya watumishi.

B. MAPATO

1. Kodi-Ushuru wa mazao
   Mapato kutokana na kodi mbalimbali kama ushuru wa mazao yameongezeka kutoka Sh 2,904,991,683 mwaka 2014/2015 mpaka Sh 3,395,868,925 kwa msimu wa 2015/2016 kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa zao la korosho pamoja na bei ya korosho.

2. Ada, faini, adhabu na leseni
   Mapato kutokana na vyanzo hivi yameongezeka kutoka Sh 78,412,590 mwaka 2014/2015 mpaka Sh 157,985,914 mwaka 2015/2016, ongezeko ili kubwa limetokana na sehemu kubwa ya uchangiaji wa huduma za afya (cost sharing).

3. Ruzuku ya kawaida
   Mapato yanayotokana na fedha za ruzuku zilizotoka serikalini kwa matumizi ya kawaida yameongezeka kutoka Shs 20,868,508,634 kwa mwaka 2014/2015 mpaka Shs 23,880,860,1991 mwaka 2015/2016 kutokana na ongezeko la mishahara na

watumishi wapya walioajiliwa huku ruzuku ya matumizi mengineyo ikipokelewa ya miezi minne tu kwa mwaka wote.

4. Thamani ya rasilimali zilizotumika
   Hii ni sehemu ya uchakavu wa majengo, mitambo na vifaa ambayo inajumuishwa kama sehemu ya mapato kwa kila mwaka baada ya kutumika hiyo rasilimali Kwa mwaka 2015/2016 thamani ya rasilimali iliyotumika ilikuwa Sh 1,089,627,387.

C. MATUMIZI

1. Vibarua, Mishahara na Maslahi ya mwajiriwa
   Malipo ya mishahara na maslahi ya watumishi yameongezeka kutoka Sh **16,479,166,477** mwaka **2014/2015** mpaka sh **20,338,108,054** ongezeko hili limetokana na viwango vipya vya mishahara ya serikali pamoja na ajira mpya.

2. Ununuzi wa vifaa na gharama za kujikimu kwa wafanyakazi
   Ununuzi wa vifaa na gharama za kujikimu kwa watumishi umeongezeka kutoka sh. **2,164,045,863** mwaka **2014/2015** mpaka sh. **2,339,482,424** mwaka **2015/2016**. Hii inasababishwa na kuongezeka kwa matumizi ya shajala hususani matumizi ya karatasi na wino kwa matumizi ya mfumo wa Epicor 09 na ongezeko la kima cha posho ya kujikimu na posho ya kazi saa za ziada kwa watumishi.

3. Gharama za matengenezo
   Matumizi ya gharama za matengenezo ni pamoja na matengenezo ya barabara na magari na ununuzi wa mafuta ya kuendeshea mitambo, magari na pikipiki ambayo yamepungua kutoka sh. **1,427,125,615** mwaka **2014/2015** mpaka sh. **934,994,727** mwaka **2015/2016**. Hii inatokana na matumizi ya miradi ya barabara kupungua kutokana na serikari kuu kutoleta fedha zote kulingana na makisio

4. Ruzuku na michango ya kuchangia jamii
   Kiasi kimepungua kutoka sh **2,073,423,507** mwaka **2014/2015** hadi Sh **1,782,194,325** mwaka **2015/2016**. Hii imetokana na halmashauri kutopeleka fedha za michango ya maendeleo vijijini kutokana na utekelezaji wa maagizo ya ujenzi wa maabara na utengenezaji wa madawati.

5. Uchakavu wa mitambo na vifaa
   Ni sehemu ya makadirio ya uchakavu wa majengo, mitambo na vifaa kwa mwaka (depreciation expenses). Kumekuwa na ongezeko la sh. **160,532,003** (Sh. **1,040,487,743** mwaka **2012/2015** hadi Sh. **1,201,019,746** mwaka **2015/2016**) kutokana na kukamilika kwa miradi mbalimbali ambayo ilikuwa katika hatua za utekelezaji mwishoni mwa mwaka uliopita na ununuzi wa vitendea kazi vipya.

Changamoto

- Serikali Kuu kuchelewa au kutoleta kabisa fedha za maendeleo kunachangia miradi mingi inayofadhiliwa na serikali kutokamilika/kutofanyika kwa wakati uliokusudiwa

- Halmashauri kwa mwaka wa fedha ulioishia **Juni 2016** imeshindwa kutekeleza miradi yake mingi kulingana na makisio kutokana na kutekeleza agizo la kutengeneza madawati ya shule za msingi na sekondari.
- Halmashauri kuendelea kupokea ushuru wa zao la korosho kutokana na bei dira badala ya bei ya soko (farm gate price) kwa mujibu wa kifungu cha 7(1)(g) cha sheria ya fedha za Serikali za Mitaa, Namba 09 ya mwaka 1982 inavyotaka imesababisha Halmashauri kukosa zaidi ya bilioni tatu kwa mwaka wa fedha ulioisha ambazo zingeweza kutekeleza miradi mingi ya maendeleo.

Taarifa ilipokelewa.

YALIYOJITOKEZA

Mwenyekiti alitoa ufafanuzi kuwa taarifa ya hesabu za mwisho kwa mwaka wa fedha husika inatakiwa ijadiliwe katika Baraza maalum ila sheria haikutaja kuwa ni lazima ipitiwe na Kamati ya Fedha, Mipango na Uongozi.

SUALA LA WADAIWA

Mjumbe alihoji juu ya wadaiwa wa fedha wa Halmashauri. Ilielezwa kuwa kiasi kikubwa cha wadaiwa ni vyama vya msingi na kueleza kuwa tayari vyama hivyo vimeahidi kulipa deni lao ambalo ni shilingi 1.6n bilioni.

HITIMISHO

Mwenyekiti alieleza kuwa mpango wa kuhakikisha vyama vya msingi vinalipa madeni yao utawasilishwa kwenye vikao vya mwezi Oktoba, 2016

SUALA LA KUTOZA USHURU WA ZAO LA KOROSHO KWA BEI YA SOKO

Mjumbe alihoji juu ya upotevu wa mapato kwa kutumia bei dira kutoza ushuru wa zao la korosho badala ya kutumia bei ya soko na kuhoji juu ya mikakati ya kuokoa mapato hayo kwa msimu wa 2016/2017. Katibu alieleza kuwa suala hilo bado halijapata ufumbuzi. Mweka Hazina (W) alieleza kuwa suala hilo ni changamoto kubwa kwani sheria inazitaka Halmashauri kutoza ushuru kwa bei ya soko badala ya mfumo wa sasa wa kutoza ushuru kwa kutumia bei dira.

Mwenyekiti alieleza kuwa kuna changamoto katika kupata ufumbuzi wa utozaji wa ushuru wa zao la korosho kwa kueleza kuwa Mkutano wa Wadau wa korosho umeridhia utozaji wa ushuru kwa kutumia bei dira na kueleza kuwa uwakilishi wa Wilaya zinazozalisha zaidi korosho kama Tandahimba kwenye mkutano huo ni mdogo hali inayopelekea kutokuwa na nguvu katika kufanya maamuzi.

HITIMISHO

Kikao kiliagiza Mwanasheria afungue kesi mahakamani kuomba tafsiri ya sheria ya utozaji ushuru ili kupata ufafanuzi utakaosaidia Halmashauri kutoza ushuru kwa bei ya soko badala ya kutoza kwa bei dira.

SUALA LA KUTOTOLEWA KWA FEDHA ZA RUZUKU YA MAENDELEO
Mjumbe alihoji juu ya kutotolewa kwa fedha za ruzuku ya maendeleo kutoka serikali kuu. Mwenyekiti alieleza kuwa majibu yalishatolewa na serikali kuwa ilikuwa inapanga uongozi mpya ili fedha hizo zitakapotolewa zitumike kwa matumizi sahihi.

Taarifa ilipokelewa.

MUHT. NA. 03/2016/2017- KUFUNGA KIKAO
Katibu aliwashukuru wajumbe na kisha alimkaribisha Mwenyekiti afunge kikao. Mwenyekiti aliwahimiza madiwani kupambana na wanunuzi wa korosho wasio rasmi (kangomba) kwani wanasababisha kushuka kwa bei ya korosho mnadani na pia wanaikosesha Halmashauri mapato. Alihimiza pia uhamasishaji wa wananchi kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) na kuhamasisha wakulima kufungua akaunti zitakazotumika kuingiza malipo yao ya mauzo ya korosho na kusisistiza kuwa wakulima watalipwa fedha zao zote kwa awamu moja hivyo hakutakuwa na malipo ya majaliwa na pia wahamasishwe kuchangia pembejeo. Kikao kilifungwa saa 07:33 mchana.